BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2015

## 021 KISWAHILI

**(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni)**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2015

# 021 KISWAHILI

**(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni)**

Kimechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624, Dar es Salaam
Tanzania

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2016**

Haki zote zimehifadhiwa

# YALIYOMO

DIBAJI ........ iv
1.0 UTANGULIZI ........ 1
2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI ........ 1
2.1 Sehemu A: Ufahamu na Ufupisho ........ 2
2.1.1 Swali la 1: Ufahamu ........ 2
2.1.2 Swali la 2: Ufupisho ........ 5
2.2 Sehemu B: Sarufi na Matumizi ya Lugha ........ 7
2.2.1 Swali la 3: Matumizi ya Lugha ........ 7
2.2.2 Swali la 4: Matumizi ya Lugha ........ 9
2.2.3 Swali la 5: Uundaji wa Maneno ........ 13
2.2.4 Swali la 6: Sarufi – Dhima za Mofimu ........ 16
2.2.5 Swali la 7: Sarufi - Uundaji wa Maneno ........ 20
2.3 Sehemu C: Uandishi ........ 22
2.3.1 Swali la 8 Uandishi wa Matangazo ya Kibiashara ........ 22
2.3.2 Swali la 9: Uandishi wa Kadi ya Mwaliko ........ 24
2.4 Sehemu D: Maendeleo ya Kiswahili ........ 27
Swali la 10: Maendeleo ya Kiswahili ........ 27
2.5 Sehemu E: Fasihi kwa Ujumla ........ 33
2.5.1 Swali la 11: Utungaji wa Kazi za Fasihi Simulizi ........ 33
2.5.2 Swali la 12: Uhakiki wa Ushairi ........ 38
2.5.3 Swali la 13: Uhakiki wa Riwaya ........ 45
2.5.4 Swali la 14: Uhakiki wa Tamthiliya ........ 50
2.5.5 Swali la 15: Utungaji wa Kazi za Fasihi Simulizi ........ 55
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA ........ 60
4.0 HITIMISHO ........ 61
5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ........ 62
KIAMBATANISHO A ........ 63
KIAMBATANISHO B ........ 64

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linayo furaha kutoa taarifa ya watahini kuhusu ufaulu wa watahiniwa katika Mtihani wa Kuhitimu Kidato cha Nne kwa somo la Kiswahili. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu katika mtihani wa somo hilo kwa wanafunzi, walimu, wazazi, watunga sera na jamii kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho ambayo, pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa yale ambayo mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa walipokuwa katika elimu ya Sekondari.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vizuri au vibaya katika mtihani wao. Taarifa inaonesha baadhi ya sababu zilizofanya watahiniwa wengi kupata alama za juu katika majibu yao. Sababu hizo ni kama vile kuelewa maelekezo na mahitaji ya swali, kuwa na maarifa na ujuzi katika kujieleza kwa ufasaha na kuwa na uelewa wa mada mbalimbali za somo la Kiswahili. Aidha, taarifa hii inaonesha sababu zilizofanya watahiniwa wachache kutokufanya vizuri kwenye baadhi ya maswali kama vile kukosa maarifa na ujuzi katika kujieleza kwa ufasaha kuhusu dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili. Mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa shule, walimu na wanafunzi kupata mbinu mwafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania litapenda kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na umma kwa ujumla ambayo yatatumika katika kuboresha taarifa za watahini zitakazofuata.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, walimu na wengine wote waliohusika katika kutayarisha taarifa hii. Tunapenda vilevile kutoa shukrani zetu za pekee kwa wafanyakazi wa Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano walioshiriki katika uchambuzi wa takwimu zilizotumika katika taarifa hii.



Dr. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua ufaulu wa Watahiniwa wa Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) Mwaka 2015 kwa somo la Kiswahili. Mtihani huo ulikuwa na maswali 15 yaliyogawanyika katika sehemu A, B, C, D na E kwa kuzingatia mada za *Ufahamu na Ufupisho*, *Sarufi na Matumizi ya Lugha*, *Uandishi*, *Maendeleo ya Kiswahili* na *Fasihi kwa Ujumla*.

Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A, B na D, swali moja (1) kutoka sehemu C na maswali matatu (3) kutoka sehemu E. Swali la 15 lilikuwa ni la lazima.

Mtihani wa somo la Kiswahili kwa Mwaka 2015 ulifanywa na watahiniwa **384,014** kati ya watahiniwa hao, waliofaulu ni **298,105** sawa na asilimia **77.63** ya watahiniwa wote waliofanya mtihani, yaani waliopata daraja A hadi D. Kiwango hicho cha ufaulu kwa ujumla kilikuwa ni cha juu ikilinganishwa na kilivyokuwa mwaka 2014. Aidha, asilimia ya waliofaulu kwa mwaka 2014 ilikuwa **69.66** ambayo ni ya chini kwa asilimia 7.97 ikilinganishwa na asilimia ya waliofaulu Mwaka 2015. Sehemu inayofuata inafafanua tathmini ya kila swali.

## 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

Katika sehemu hii uchambuzi wa kina kwa kila swali utafanyika kwa kuonesha maswali yaliyofanyika vizuri na yale yaliyofanyika vibaya na kutoa sababu zilizosababisha kuwepo kwa ufaulu mzuri au mbaya katika maswali hayo. Aidha, vielelezo vioneshavyo maswali yaliyofanyika vizuri na yale yaliyofanyika vibaya vitaambatishwa ili kushadidia maelezo ya uchambuzi wa ufaulu huo.

Viwango vya ufaulu vimewekwa katika makundi matatu kwa kuzingatia asilimia ya watahiniwa waliopata wastani wa alama 30 au zaidi katika kila swali. Wastani wa ufaulu ukiwa asilimia 0 hadi 29 ni ufaulu hafifu ambao unawakilishwa na rangi nyekundu, asilimia 30 hadi 44 ni ufaulu wa wastani na unawakilishwa na rangi ya njano na asilimia 45 hadi 100 ni ufaulu mzuri ambao unawakilishwa na rangi ya kijani.

## 2.1 Sehemu A: Ufahamu na Ufupisho

### 2.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali lilihusu mada ya *Ufahamu* na lililenga kupima maarifa. Swali lilikuwa na vipengele vitano vilivyobeba jumla ya alama sita (6). Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yaliyofuata kutoka katika kifungu hicho. Maswali hayo yaligawanyika katika kipengele (a) hadi (e) ambapo kipengele (a) kiligawanyika katika sehemu (i-v) na kila kipengele kilikuwa na alama $^{1}/_{2}$. Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa aeleze maana ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari. Maneno hayo yalikuwa (i) *Utashi* (ii) *Hamaki* (iii) *Kiimla* (iv) *Mrama* na (v) *Muhali*.

Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa ataje mambo mazuri mawili yatokanayo na uwepo wa katiba katika nchi na kilikuwa na alama 1.

Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa atoe ufafanuzi kuhusu sababu zilizomfanya mwandishi kusema kuwa katiba hutumiwa kama sera kwa masilahi ya watawala. Kipengele hiki kilikuwa na alama $^{1}/_{2}$.

Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa aelezee hofu aliyokuwa nayo mwandishi dhidi ya vijana kuhusu katiba na kilikuwa na alama 1. Kipengele (e) kilimtaka mtahiniwa aandike kichwa cha habari aliyoisoma kisichozidi maneno matano na kilikuwa na alama 1.

Swali lilijibiwa na asilimia 96.1 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani, ambapo kati yao asilimia 81.2 walijibu vizuri maswali ya vipengele (a) hadi (e) na kupata alama 2 hadi 6. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 38.1 walipata alama 2 hadi $2^{1}/_{2}$. Watahiniwa hao walipata ufaulu wa wastani kwa kuwa walitoa majibu sahihi kwa vipengele viwili na kushindwa vipengele vitatu. Asilimia 58.8 ya watahiniwa walipata alama 3 hadi 6. Watahiniwa hao waliweza kujibu vipengele vitatu hadi vitano kwa usahihi.

Kielelezo 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu maswali ya vipengele (a) hadi (e) kwa usahihi.

**Kielelezo 1.1**

1(a) Utashi – Ni hali ya kujitambua au kutambua jambo au mambo mbalimbali mabaya kwa mazuri.
Hamaki – Ni hali ya kukasirika
Kiimla – Ni utaratibu unaoendeshwa na watu baadhi pasi kushirikisha wananchi kwa maana nyingi na mwandishi amemaanisha nchi zenye udikiteta.
Mrama – Ni hali ya kupoteza mwelekeo.
Muhali – Ni kutowezekana

(b) i) Katiba huelekeza wajibu wa kila mwananchi kwa taifa lake na wajibu wa viongozi walio madarakani kwa wananchi au raia.
ii) Katiba huonesha na kuainisha haki ambazo kila raia anastahili kupata na taratibu za kufuata katika kudai au kupewa haki hizo.

(c) Kwa sababu katiba zisizoshirikisha maoni ya wananchi huwa ni kama katiba za viongozi wa ngazi za juu na zipo kwa ajili ya maslahi ya viongozi tu.


1(d) Mwandishi anahofu kwa sababu vijana walio wengi hubumbwa na watawala kutokana na ufinyu wa uelewa wa vijana kuhusu katiba na hii inatokana na kutowajibika kujua katiba.

(e) KATIBA YA NCHI!

Kielelezo 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufuata matakwa ya swali na kutoa majibu sahihi katika vipengele vyote vya swali.

Watahiniwa wachache tu (18.8%) walishindwa kujibu vizuri swali hili, kwa sababu baadhi yao walishindwa kueleza maana ya maneno waliyopewa katika kifungu cha habari. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu kama ifuatavyo; (a) (i) *utashi* ni *amani au furaha* (ii) *Hamaki ni vurugu au fujo* (iii) *Mrama ni kwenda umbali mrefu au mbali na hapo* na (iv) *Muhali ni mapema* majibu ambayo sio sahihi. Aidha, mtahiniwa huyo hakujibu kwa usahihi vipengele (b) na (c) isipokuwa kipengele (e) pekee ndicho alichoweza kujibu kwa usahihi kama Kielelezo 1.2 kinavyoonesha.

**Kielelezo 1.2**



1 (a) Kutoa maana ya maneno yale yaliyokolezwa wino kama yalivyotumika katika habari
i/ Utashi, ni amani au furaha
ii/ Hamaki, vurugu au fujo
iii/ Kiimla, kisheria au Maalum
iv/ Mrama, kwenda umbali mrefu au mbali na hapo
v/ Muhali, Ni mapema
b Kutaja mambo mazuri mawili yanayokanayo na uwepo wa katiba katika nchi
i/ Utamaduni wa kidemokrasia
ii/ Nchi zenye utaratibu wa kiima au kisheria
c Mwandishi anaposema Sera kwa maslahi ya watawala ina maana, kujiendeleza kimaisha katika jamii
d
e Kuandika kichwa cha habari, ni Katiba

Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuweza kujibu kwa usahihi vipengele vinne vya swali, mtahiniwa huyo alijibu kwa usahihi kipengele (e) tu.

### 2.1.2 Swali la 2: Ufupisho

Swali lilihusu mada ya *Ufahamu na Ufupisho* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutumia maarifa aliyopata ili kufupisha habari. Swali lilikuwa na alama 4 na lilimtaka mtahiniwa kufupisha habari aliyosoma kwa maneno yasiyopungua mia moja (100). Swali lilijibiwa na asilimia 83.7 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani.


Asilimia 89.3 ya watahiniwa waliofanya swali hili walijibu vizuri, kati yao asilimia 81.7 walipata alama 2 hadi 4. Aidha, asilimia 7.6 walipata ufaulu wa wastani na hivyo kupata alama $1^1/_2$. Watahiniwa wachache (10.7%) walishindwa kujibu vizuri na kupata alama 0 hadi 1. Chati Na. 1 inafafanua vizuri ufaulu huo.




**Chati Na 1: Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia**.

Watahiniwa wengi (81.7%) walizingatia matumizi sahihi ya alama za uandishi, lugha sanifu, mpangilio wa mawazo wenye mantiki, uzingatiaji wa idadi ya maneno kama ilivyoelekezwa katika swali na utumiaji maneno tofauti bila kupotosha kiini cha habari ya awali. Kielelezo 2.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kuandika ufupisho kwa kutumia maneno yake mwenyewe bila kupotosha kiini cha habari ya awali.

**Kielelezo 2.1**


2.

UMUHIMU WA KATIBA.

Mwenendo mzuri wa kuheshimu na kufuatwa na watu katika jamii fulani au eneo fulani, ni jambo lenye kupendeza na kufurahisha. Utaratibu na uongozaji wa mambo mbalimbali ni muhimu katika jamii.

Mjumuiko wa kanuni, taratibu uliokubaliwa kisheria hufahamika kama katiba. Katiba hutumika kuendesha mambo mbalimbali katika nchi zinazofuata mfumo wa kidemokrasia.

Katiba ina umuhimu mkubwa kwani inalinda haki ya kila raia, huelekeza wajibu wa kila mwanajamii, pia hutoa utaratibu wa jinsi ya kuchagua na kuwapata viongozi mbalimbali. Katiba ni muhimu kwa manufaa ya jamii kwa ujumla.

Ni vizuri kufahamu katiba za nchi zetu, kwa lengo na madhumuni ya kutambua haki zetu ili kufikia malengo ya kidemokrasia.

Kielelezo 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutumia maneno yake mwenyewe bila kupotosha kiini cha habari kwa kuzingatia mtiririko wa mawazo wenye mantiki, matumizi ya lugha sanifu pamoja na idadi ya maneno kama alivyoelekezwa.

Aidha, watahiniwa wachache (10.7%) walipata alama 0 hadi 1 kwa kuwa hawakuzingatia kanuni za uandishi na kanuni za ufupisho kama vile kutumia maneno yao bila kupotosha kiini cha habari ya awali, kuzingatia mtiririko wa mawazo wenye mantiki, kufuata taratibu za uandishi, matumizi ya lugha sanifu na idadi ya maneno kulingana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika ufupisho usiozingatia mada ya katiba ambayo ndiyo kiini cha kifungu cha habari walichopewa. Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli

ya majibu ya mtahiniwa ambaye aliandika ufupisho ambao unazungumzia kuhusu ustaarabu tofauti na kichwa cha habari waliyopewa.

**Kielelezo 2.2**

Kufupisha habari hii kwa maneno yasiyopungua (100).

Ustarabu ni jambo jema ambalo hupendwa na kila
jamiiyenye ustaraabu hapa duniani. Kila jamii yenye usta
rabu mambo yake huendeshwa kwa kuzingatia kanuni
na taratibu zinazoeleweka. Maamuzi na mafanikio mba
limbali miongoni mwa wanajamii hutolewa bila kutaf
akari wa ~~kukiuka~~ kupuka kanuni na taratibu hizo hu
iongoza jamii kufikia upeo wake.

Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubaini mawazo makuu katika habari aliyoisoma. Ufupisho wake umejikita zaidi katika *ustaarabu* badala ya umuhimu wa katiba hivyo kupotosha ujumbe uliopo katika habari ya awali.

## 2.2 Sehemu B: Sarufi na Matumizi ya Lugha


### 2.2.1 Swali la 3: Matumizi ya Lugha

Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima matumizi ya lugha. Aidha, swali lilimtaka mtahiniwa kutaja aina mbili za makosa yanayoweza kujitokeza katika kutumia lugha ya Kiswahili na kutoa mifano ya sentensi mbili kwa kila kosa. Swali lilikuwa na jumla ya alama 5.

Asilimia 78.8 ya watahiniwa wote waliojibu swali walishindwa kujibu swali hili vizuri kwani hawakuweza kutaja aina mbili za makosa yanayoweza kujitokeza katika kutumia lugha ya Kiswahili, badala yake walitaja makosa ambayo hayahusiani na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Miongoni mwao, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yanayohusu makosa ya kisheria kama vile *makosa ya jinai* na

*makosa ya madai* kisha aliandika mifano ya sentensi kama hivi: *Unatuhumiwa kuiba kuku, Unashtakiwa kwa kosa la kubaka* na *Unashtakiwa kwa kosa la kudai ushuru* sentensi ambazo zinaendana na makosa aliyotaja lakini sio sahihi kuhusiana na mada ya *Matumizi ya Lugha* ya Kiswahili. Kielelezo 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alijibu swali katika muktadha wa kisheria na siyo makosa kulingana na matumizi ya lugha ya Kiswahili.

**Kielelezo 3.1**


3. i/ makosa ya jinai
ii/ Makosa ya madai.

Makosa ya jinai
mfano. unatuumiwa kwa kuiba kuku
unashtakiwa kwa kosa la kubaka


Makosa ya madai
mifano. unashtakiwa kwa kosa la kudai ushuru
unashtakiwa kwa kosa la kuomba msaada.

Kielelezo 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyechanganya dhana ya matumizi ya lugha kwa ujumla na matumizi ya lugha katika mkabala wa kisheria, hivyo kujibu kinyume na maelekezo ya swali.

Asilimia 22.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili waliweza kujibu vizuri na kupata alama zaidi ya wastani. Miongoni mwao, watahiniwa wachache sana (1.6%) waliweza kupata alama 3 hadi 5. Watahiniwa hao, waliweza kutaja makosa ya kisarufi na makosa ya kimantiki katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kueleza makosa ya kisarufi alitoa mfano wa sentensi *Juma ugali anakula* badala ya *Juma anakula ugali*. Sentensi ya pili mtahiniwa huyo aliandika *Juma amenunua fyatu* badala ya *Juma amenunua viatu.* Aidha, katika makosa ya kimantiki mtahiniwa aliandika sentensi kama vile *Chai imeingia nzi* badala ya *Nzi ameingia kwenye chai* na mfano wa pili kwenye kosa hilo mtahiniwa aliandika *Nyumba imeingia nyoka* badala ya *Nyoka ameingia kwenye nyumba.* Kielelezo

3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 3.2**


3. (a) Makosa ya Kisarufi.
Makosa ya Kisarufi yamegawanyika katika vipengele mbalimbali ambavyo kuna makosa ya kimuundo, makosa ya kimatamshi, makosa kimtindo na kuongeza vitamkwa.
Mfano.
Juma ugali anakula badala ya Juma anakula ugali.
ii) Juma amenunua fyatu badala ya Juma amenunua viatu.

3. (b) Makosa ya Kimantiki
Mfano:
i) Chai imeingia nzi badala ya nzi ameingia kwenye Chai
ii) Nyumba imeingia nyoka badala ya nyoka ameingia kwenye nyumba.


Kielelezo 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuonesha makosa ya kisarufi na ya kimantiki kwa usahihi.

### 2.2.2 Swali la 4: Matumizi ya Lugha

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha* na lililenga kupima maarifa ya utumiaji wa lugha. Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kutoa maana ya rejesta na kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kutaja mambo muhimu matatu yanayomwongoza mtumiaji wa lugha katika kuteua rejesta na kutoa mfano mmoja kwa kila jambo. Swali hili lilikuwa na alama 5.

Asilimia 67.4 ya watahiniwa walijibu swali hili vizuri, miongoni mwao, asilimia 35.9 walijibu vizuri zaidi na kupata alama $2^1/_2$ hadi 5. Watahiniwa hao waliweza kueleza maana ya rejesta na kutaja mambo matatu muhimu yanayomwongoza mtumiaji wa lugha katika uteuzi wa rejesta. Mambo hayo matatu ni kama vile*; mandhari au mazingira yaliyopo, uhusiano uliopo baina ya watumiaji na mada ya mazungumzo*. Kielelezo 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutaja mambo matatu muhimu yanayomwongoza mtumiaji wa lugha katika uteuzi wa rejesta.

**Kielelezo 4.1**


4. a) Rejesta
ni mtindo wa lugha unaochimiwa na kundi la watu fulani ili kuleta maana baina yao na kutumiwa katika mazungumzo.

b). Mambo muhimu katika uteuzi wa rejesta.
• Mandhari / Mazingira yaliyopo.
Mteuzi wa rejesta anatakiwa kuangalia

4. mazingira yapi yanayomruhusu ili kukwepa malumbano baina ya watu.
Mfano:-Hospitalini
Mbili asubuhi, mchana na usiku.
- Sokoni
Maembe matatu kwa Shilingi mia tano.

4. • Uhusiano uliopo baina ya wahu.

Mtumiaji wa lugha anatakiwa aangalie uhusiano uliopo baina ya wahu hao ili rejesta hiyo iweze kueleweka na kuepusha magombano.

Mfano: kijana kwa kijana mwenzake/ - mitaani.

- Aisee mshkaji yule ticha kanichapa eti nimeiba simu yake.

mshkaji - mwalio rafiki

ticha - mwalimu

kanichapa - kanichongea uongo.

• Mada ya mazungumzo.

Mtumiaji wa lugha aaingalie ni mada ipi inaongelewa ili kuteua rejesta ambayo inafaa kutumika.


Mfano: Biashara

• Mashati saba kwa nyekundu mbili na punguzo la bei

Kielelezo 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetaja mambo matatu muhimu yanayomwongoza mtumiaji wa lugha katika uteuzi wa rejesta na kutoa mifano maridhawa.

Hata hivyo, asilimia 31.6 ya watahiniwa walipata alama $1^1/_2$ hadi 2. Watahiniwa hao hawakuweza kueleza maana ya rejesta ijapokuwa waliweza kutaja mambo mawili ya kumwongoza mtumiaji wa lugha katika uteuzi wa rejesta na pia waliweza kutoa baadhi ya mifano iliyo sahihi. Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa kiwango cha wastani.

**Kielelezo 4.2**



4 (a) Rejesta ni

(b) - Mahali / sehemu

Kutokana na mahali alipo mtu panaweza kumwongoza mtumiaji wa lugha katika uteuzi wa rejesta kama mtaani

Mfano:

Mtu awapo kanisani

- Bwana Yesu asifiwe

Amina!

- Umri baina ya watu.

Kutokana na uteuzi wa rejesta zipo lugha za vijana ambapo watu wazee hawataweza vyema kutumia.

Mfano:

Oya, vipi? mshkaji utaondoka [illegible]

Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza maana ya rejesta lakini aliweza kutaja mambo mawili kwa usahihi na hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, asilimia 32.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walishindwa kueleza maana ya rejesta na kutaja mambo matatu muhimu yanayomwongoza mtumiaji wa lugha katika uteuzi wa rejesta na hivyo kupata alama chini ya wastani. Miongoni mwao, asilimia 14.7 walipata alama 0 kwa sababu walichanganya dhana ya rejesta na tafsida, hivyo walielezea rejesta kuwa ni *maneno yatumikayo katika sehemu ili kupunguza ukali wa maneno katika mazungumzo baina ya*

*watu*. Aidha, watahiniwa wengine katika kipengele (b) kilichomtaka mtahiniwa ataje mambo matatu muhimu yanayomwongoza mtumiaji wa lugha katika uteuzi wa rejesta, walitoa hoja zinazofafanua sifa za rejesta kwa mfano, (i) *Kufupisha maneno* (ii) *Kumfanya mtu kuelewa kwa haraka* na (iii) *Kuficha jambo.* Majibu haya siyo mambo matatu muhimu yanayomwongoza mtumiaji wa lugha katika uteuzi wa rejesta. Kielelezo 4.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetaja sifa za rejesta badala ya kutaja mambo matatu muhimu yanayomwongoza mtumiaji wa lugha katika uteuzi wa rejesta.

**Kielelezo 4.3**

| | |
|---|---|
| 4a) | Rejesta-Ni maneno yatumikayo katika sehemu ili kupunguza ukali wa maneno nakatika kikundi cha watu. |
| | |
| b). | i) Kufupisha maneno |
| | Mfano: Nipatie wali kuku |
| | |
| | ii) Kumfanya mtu kuelewa haraka |
| | |
| | iii) Kuficha jambo |
| | Mfano: Yule ni mzuri |

Kielelezo 4.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza maana ya tasfida na kutoa jibu ambalo ni kinyume na matakwa ya swali katika vipengele vyote.

### 2.2.3 Swali la 5: Uundaji wa Maneno


Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kuunda dhana na lilikuwa na alama 5.

Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika neno moja lenye maana sawa na maelezo aliyopewa katika kila sentensi. Maelezo hayo yalikuwa na kipengele (a) hadi (e) kama ifuatavyo:

*(a)* *Mtu anayechunguza uhalifu*
*(b)* *Ng'ombe dume aliyehasiwa*
*(c)* *Chombo cha usafiri kinachopita juu ya vyuma*
*(d)* *Mti unaozaa matunda yanayotengenezwa kinywaji cha kahawa.*
*(e)* *Sehemu ndogo ya nchi iliyochongoka na kuzungukwa na bahari katika sehemu zake tatu*

Asilimia 56.3 ya watahiniwa walijibu vizuri kwa sababu swali lilitoka katika mazingira yaliyowazunguka na mambo yaliyoulizwa huwa yanajitokeza katika jamii na hata katika vyombo mbalimbali vya habari huwa yanazumgumziwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kuandika neno moja lenye maana sawa na maelezo aliyopewa katika kila kipengele kama Kielelezo 5.1 kinavyoonesha.


**Kielelezo.5.1**


5. Kua ndika neno moja lenye maana sawa na maelezo ya sentensi;
(a) Mtu anaye chunguza uhalifu- Mpelelezi.
(b) Ng'ombe dume aliye hasiwa- Maksai.
(c) Chombo cha usafiri kinachopita juu ya vyuma-Treni.
(d) Mti unaozaa matunda yanayo tengeneza kinywaji cha kahawa - Mbuni.
(e) Sehemu ndogo ya nchi iliyochongoka na kuzu-ngukwa na bahari katika sehemu zake tatu- Rasi.

Kielelezo 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuandika neno moja lenye maana sawa na maelezo aliyopewa katika kila sentensi na kupata alama zote.

Aidha, asilimia 31.6 ya watahiniwa walijibu kwa kiwango cha wastani kutokana na kujua maneno mawili yaliyokuwa na maana sawa na maelezo ya sentensi mbili tu alizopewa na kushindwa kutoa maana ya sentensi nyingine tatu kati ya sentensi tano alizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kueleza maana mbili kama Kielelezo 5.2 kinavyoonesha.


**Kielelezo 5.2**


5 a) Mpelelezi.
b) Maksai.
c)
d)
e)

Kielelezo 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye aliweza kujibu vipengele viwili vya 5(a) na 5(b) pekee.

Hata hivyo, asilimia 43.4 ya watahiniwa walipata alama chini ya wastani. Miongoni mwa watahiniwa hao asilimia 17.8 walipata alama 0. Watahiniwa hao walichanganya dhana na hivyo kushindwa kueleza neno lenye maana sawa na maelezo waliyopewa katika kila sentensi, badala yake waliandika kinyume na maelekezo ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kuandika neno moja lenye maana sawa na maelezo ya kipengele (a) *Mtu anayechunguza uhalifu* aliandika *Uhalifu unachunguzwa na mtu*. Kipengele (b) *Ng'ombe dume aliyehasiwa* aliandika *Aliyehasiwa ni ng'ombe dume* na katika kipengele (c) *Chombo cha usafiri kinachopita juu ya vyuma* aliandika *Vyuma vinavyopita juu ya chombo cha usafiri*. Majibu haya yalionesha kauli taarifa badala ya kuandika neno moja linalotoa maana ya maelezo katika kila sentensi. Kielelezo 5.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambayo hayakukidhi maelekezo ya swali.

**Kielelezo 5.3**


5 (a) Mtu anayechunguza uhalifu
- Uhalifu unachunguzwa na mtu
(b) Ng'ombe dume aliyohasiwa
- aliyohasiwa ni ng'ombe dume
(c) Chombo cha usafiri kinachopita juu ya vyuma
- Vyuma vinavyopita juu ni chombo cha usafiri
(d) Mti unaozaa matunda yanayotenga-nzwa kinywaji cha kahawa
- Kinywaji chaotoka kutokana na matunda
(e) Sehemu ndogo ya nchi iliyochongoka na kuzunguka na bahari katika sehemu tatu
- Sehemu iliyochongoka imezungukwa na bahari


Kielelezo 5.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyechanganya dhana kwa kuandika kauli taarifa badala ya kutoa neno lenye maana sawa na maelezo aliyopewa.

### 2.2.4 Swali la 6: Sarufi – Dhima za Mofimu

Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lilimtaka mtahiniwa kueleza dhima za mofimu *li* kama ilivyotumika katika sentensi tano alizopewa. Swali lilikuwa na alama 5 na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kutumia maarifa aliyonayo kubainisha dhima za mofimu.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya na watahiniwa wengi kutokana na asilimia 93.1 ya watahiniwa


wote waliojibu swali hili kushindwa kueleza dhima za mofimu *li* kama ilivyotumika katika sentensi walizopewa hivyo kupata alama 0 hadi 1. Asilimia 5.1 walipata alama $1^1/_2$ hadi 2 ambazo ni alama za wastani. Aidha, asilimia 1.8 pekee ndio waliojibu vizuri zaidi na kupata alama $2^1/_2$ hadi 5. Chati Na 2 inaonesha ufaulu huo wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na.2: Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia**

Asimia 67.5 kati ya asilimia 93.1 ya watahiniwa waliojibu vibaya walipata alama 0. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuhusu maana na dhima ya mofimu. Baadhi ya watahiniwa hao walieleza dhima za mofimu *li* kwa kuandika sentensi ambazo hazina uhusiano na swali waliloulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kipengele (a) aliandika *dhima ya mofimu li ni kuunganisha maneno katika sentensi.* Katika kipengele (b) aliandika *mofimu li imetumika kuleta maana iliyo sahihi katika sentensi*, kipengele (c) aliandika *mofimu li imetumika kuunganisha maneno*, kipengele (d) aliandika *mofimu li imetumika kuelezea juu ya jambo ambalo limetokea* na *kipengele (e)* aliandika *mofimu li imetumika kuelezea jambo*. Sentensi hizo hazikuwa majibu sahihi kama Kielelezo 6.1 kinavyoonesha.

**Kielelezo 6.1**



(6) (a) Shamba letu li kubwa sana.
*dhima ya mofimu li kuunganisha maneno katika sentensi.
(b) Walichelewa kurudi.
*katika sentensi hii mofimu li imetumika kuleta maana ili iwe sahihi katika sentensi.
(c) Tunafuatilia.
*katika sentensi hii mofimu li imetumika kuunganisha maneno.
(d) Limeharibika.
*katika sentensi hii mofimu li imetumika kueleza juu ya jambo ambalo limetokea.
(e) Shikilia.
*katika sentensi hii mofimu li imetuka kuelezea jambo.

Kielelezo 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alishindwa kueleza dhima za mofimu *li* kama ilivyotumika katika sentensi badala yake aliandika sentensi anuwai zisizokidhi matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa wachache (6.9%) waliweza kueleza dhima za mofimu *li* katika kila sentensi kwa usahihi ambapo miongoni mwao asilimia 1.8 walijibu vizuri zaidi na kupata alama $2^1/_2$ hadi 5. Baadhi ya watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya mofimu kuwa ni neno

au kipande cha neno chenye maana kisarufi, hivyo, waliweza kueleza maana ya mofimu *li* kama ilivyotumika katika sentensi kwa usahihi. Kielelezo 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza dhima za mofimu *li* katika sentensi zote kwa usahihi.

**Kielelezo 6.2**


6. (a) Li kubwa sana
·Li- Imetumika kama mofimu ya uonyeshi, jinsi shamba lilivyo.
pia kama kitenzi kishirikishi (t) kinachosaidia hali ya shamba ifahamike.

(b) Walichelewa
-li- Imetumika kama kiambishi awali kinachoonesha wakati uliopita.

(c) Tunalifuatilia.
-li- Imetumika kama kiambishi awali kionyeshacho ukubwaishaji yaani kinachofuatiliwa ni kitu kikubwa.
-li- Imetumika kama kiambishi tamati kionyeshacho kauli ya kutendea (li-a) pia ngeli ya LI-YA

(d) Limeharibika.
Li- kiambishi awali kionyeshacho ngeli ya LI-YA na upatanisho wa kisarufi katika tungo husika.

6. (e) Shikilia
-li- Kiambishi tamati kionyeshacho kauli ya kutendea yaani Shiki-li-a.

Kielelezo 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye aliweza kueleza dhima za mofimu ‘li’kama ilivyotumika katika kila sentensi kwa usahihi.

### 2.2.5 Swali la 7: Sarufi - Uundaji wa Maneno


Swali lilihusu sarufi na lililenga kupima maarifa na ujuzi wa mtahiniwa katika kuunda sentensi zenye muundo wa ukanushi na lilikuwa na jumla ya alama 5.

Asilimia 65.7 ya watahiniwa waliojibu swali walifanya vizuri na kupata alama $1^{1}/_{2}$ hadi 5. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani asilimia 55.9 ya watahiniwa waliojibu walipata alama $2^{1}/_{2}$ hadi 5. Sentensi zilizotakiwa kuandikwa katika hali ya ukanushi zilikuwa zifuatazo:

*(a)* *Ameshiba sana.*
*(b)* *Watoto wengi wanaogelea.*
*(c)* *Mvua ilinyesha kwa wingi sana.*
*(d)* *Kijana anakula chakula kingi.*
*(e)* *Mimi nasoma polepole.*

Watahiniwa waliojibu vizuri walielewa muundo wa ukanushi na viambishi (*ha* na *si*) vinavyobeba dhana ya ukanushi katika tungo. Kielelezo 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuandika sentensi alizopewa katika hali ya ukanushi.


**Kielelezo 7.1**


7 a/ Hajashiba sana
b/ Watoto wengi hawaogelei
c/ Mvua haikunyesha kwa wingi sana
d/ Kijana hali chakula kingi
e/ Mimi sisomi polepole.

Kielelezo 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuandika sentensi katika hali ya ukanushi kwa kufuata muundo wa ukanushi.

Hata hivyo, wapo watahiniwa walioshindwa kuandika sentensi walizopewa katika hali ya ukanushi. Asilimia 34.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata chini ya alama $1^{1}/_{2}$ na miongoni mwao, asilimia 25.5 walipata alama 0. Baadhi ya watahiniwa hao hawakuelewa maana ya hali kanushi na hivyo kujibu kinyume na maelekezo ya swali. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alibadilisha nafsi katika kitenzi kwa kuandika *Ameshiba sana*, *Tutashiba sana*, *Utashiba sana*. Watahiniwa wengine walibadilisha sentensi walizopewa na kuzifanya kuwa katika hali ya kuuliza. Kielelezo 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika sentensi zenye kauli ya kuuliza.

**Kielelezo 7.2**



7. Kuandika sentensi zifuatazo katika hali ya ukanushi

a) nani kakwambia ushibe sana?

b) Nani karema watoto wengi waogelee nauliza?

c) Kwanini mvua iliyonyesha kwa wingi hukuisikia?

d) we kijana kwanini unakula chakula kingi?

e) we jua mi nasoma polepole.

Kielelezo 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye badala ya kuandika sentensi katika hali ya ukanushi aliandika dhana tofauti kabisa kwa kuweka alama ya kuuliza katika sentensi hizo.


Watahiniwa wachache sana (5%) waliojibu swali hili walipata alama za wastani kutokana na kuweza kuandika sentensi mbili katika hali ya ukanushi. Baadhi ya watahiniwa hao waliweza kujibu kipengele (a) na (b) na watahiniwa wengine waliweza kujibu vipengele (d) na (e) kwa usahihi lakini vipengele vingine wakaacha nafasi zikiwa wazi bila ya kuandika chochote. Watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi kuhusu muundo ujengao sentensi katika hali ya ukanushi.

## 2.3 Sehemu C: Uandishi

### 2.3.1 Swali la 8 Uandishi wa Matangazo ya Kibiashara

Swali lilitoka kwenye mada ya *Uandishi* na lililenga kupima maarifa na ujuzi wa kuandika tangazo. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika tangazo la kibiashara la uuzaji wa gari aina ya TOYOTA CARINA. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Asilimia 92.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 67 walipata alama $4^1/_2$ hadi 10. Aidha, asilimia 25.8 walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa wachache sana (7.2%) hawakuweza kujibu swali hili vizuri hivyo kupata alama 0 hadi $2^1/_2$. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu huo wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 3: Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia**

Watahiniwa waliopata alama za juu (67%) waliweza kubaini mambo muhimu katika uandishi wa matangazo pamoja na taratibu za uandishi na matumizi ya lugha ya kibiashara. Kwa mfano, watahiniwa waliweza kubaini kuwa kichwa cha tangazo huandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari,

kiini cha tangazo huandikwa kwa maneno machache yanayotoa taarifa muhimu kama vile aina ya gari, sifa za gari linalouzwa na mahali gari hilo linapopatikana. Pia watahiniwa hao walizingatia kuwa mwisho wa tangazo huwa na jina la muuzaji na njia ya mawasiliano. Kielelezo 8.1 kinaonesha mtahiniwa aliyeandika tangazo kwa kufuata taratibu za uandishi wa matangazo.

**Kielelezo 8.1**



TANGAZO !!! TANGAZO !!!

GARI LINAUZWA.

Gari aina ya TOYOTA CARINA linauzwa lenye namba za usajili TDCY 212. Gari lina rangi nyeupe ni jipya na halijawahi kutumika, lina waranti ya mwaka mzima, TV pamoja na redio. Lina uwezo wa kutunza mafuta, linahimili umbali mkubwa sana vile vile injini ya kisasa yenye ubora

Kwa mawasiliano:
0784 33 22 81 - Mmiliki.
0652 31 21 84 - Dalali.
au
Fika Kariakoo Gerezani mtaa wa tandamti
uliza kwa Gudhah Mukosh.


Kielelezo 8.1 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa ambaye aliandika tangazo kwa usahihi na kuzingatia taratibu za uandishi wa matangazo.

Asilimia 25.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili waliweza kubaini baadhi ya mambo muhimu katika uandishi wa matangazo. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa hao waliweza kubaini sehemu tu ya kiini cha tangazo kama vile aina ya gari linalouzwa na watahiniwa wengine walitaja mahali gari linapopatikana. Aidha, watahiniwa wengine

waliweza kuandika kichwa cha tangazo na kuandika jina la muuzaji na njia ya mawasiliano. Kundi hilo la watahiniwa lilipata alama za wastani.

Aidha, asilimia 7.2 ya watahiniwa walishindwa kuandika tangazo kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa matangazo. Wapo watahiniwa walioandika namba ya swali tu bila kuandika chochote na watahiniwa wengine waliandika tangazo lenye muundo wa simu ya maandishi. Kielelezo 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika tangazo lenye muundo wa simu ya maandishi na hivyo kupata alama 0.

**Kielelezo 8.2**


8 TANGAZO TANGAZO TANGAZO!!!
GUDHAH MUKISHI ANATEUHI MTAA WA TANDAMTI
GEREZANI KARIAKOO.
ANATANGAZA KUUZWA KWA GARI YAKE AINA
YA TOYOTA CARINA.


Kielelezo 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuzingatia taratibu za uandishi wa matangazo badala yake aliandika tangazo lenye muundo wa simu ya maandishi. Hata hivyo, simu yenyewe haikukidhi vigezo vya simu ya maandishi.

### 2.3.2 Swali la 9: Uandishi wa Kadi ya Mwaliko

Swali lilitoka kwenye mada ya *Uandishi*, lilihusu uandishi wa kadi ya mwaliko na lililenga kupima maarifa na ujuzi katika uandishi. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandaa kadi ya mwaliko kwa rafiki zake ili waweze kuhudhuria mahafali itakayofanyika shuleni Kiriche tarehe 21.11.2015 na kufuatiwa na tafrija fupi itakayofanyika katika ukumbi wa Kijiji mnamo saa 10:00 jioni. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Asilimia 91.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu kwa usahihi ambapo miongoni mwao, asilimia 75.9 walipata alama 5 hadi 10 kwa kuwa waliweza kufuata taratibu zote za uandishi wa kadi ya mwaliko kama vile kuandika jina la mwandishi na anuani yake, jina la mwandikiwa/mwalikwa, lengo la mwaliko kwa ufupi, tarehe, mahali na muda wa mahafali na tafrija. Aidha, watahiniwa hao walimtaja mtu wa kurudishiwa majibu au kuwasiliana naye iwapo hataweza kuhudhuria mwaliko. Kielelezo 9.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa yaliyokidhi vigezo vya uandishi wa kadi ya mwaliko.

**Kielelezo 9.1**



9

KADI YA MWALIKO

Mimi Sili Silali ninayofuraha kubwa kukualika au kuwaalika

Anna na Juma

kwenye sherehe ya mahafali ya kumaliza kidato cha nne itakayo fanyika shuleni siku ya Jumamosi tarehe 21/11/2015 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 9:30 jioni. Na baad aye kufuatiwa na tafrija fupi itakayo fanyika katika ukumbi wa Kijiji Mnano sa 10:00 jioni.

kufika kwako ndio kufanikisha sherehe yangu

Majibu kwa wasiliane


Bw. Silali
S.L.P ~~P.O.Box~~ 220
namba za simu 0784533610

Kielelezo 9.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye aliandika kadi ya mwaliko kwa kufuata taratibu za uandishi wa kadi za mialiko kulingana na matakwa ya swali.

Asilimia 14.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 3 hadi 4 kwa kuwa baadhi yao waliweza kuandika kadi ya mwaliko kwa kuzingatia jina la mwandishi, jina la mwandikiwa, mahali ambapo tafrija itafanyikia na watahiniwa wengine waliandika tu jina la mwalikwa, tarehe, mtu wa kurudishiwa majibu, muda wa mahafali na kutokufafanua lengo la mwaliko na hivyo kupata alama za wastani.

Asilimia 8.7 tu ya watahiniwa waliojibu swali hili ndio walioshindwa kuandika kadi ya mwaliko kwa kushindwa kuzingatia taratibu za uandishi wa kadi za mialiko na hivyo kupata alama 0 hadi $2^1/_2$ kati ya alama 10 zilizotengwa kwa swali hili. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 6.6 walipata alama 0. Baadhi ya watahiniwa hao waliandika barua ya kirafiki na watahiniwa wengine waliandika barua rasmi badala ya kadi ya mwaliko. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja kwenye sehemu ya anuani ya mwandishi na anuani ya mwandikiwa katika barua rasmi aliyoandika alitumia lugha ya Kiingereza badala ya lugha ya Kiswahili. Pia alichora mchoro wa alama ya kopa kuashiria barua ya kirafiki. Kielelezo 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika barua rasmi badala ya kuandika kadi ya mwaliko.

**Kielelezo 9:2**



9\.

HANASIF SECONDAR SCHOOL,
P.O BOX 180504,
DAR-ES-SALAAM.
2-11-2015.

KIRICHE SEC. SCHOOL,
P.O. BOX 108,
DAR-ES-SALAAM.
5-11-2015.

YAH: MAHAFALI YA KUMALIZA KIDATO CHA NNE

Husika na kichwa cha habari hapo juu ni kuwa mahafali ya kumaliza kidato cha nne itakayo fanyika shuleni kwetu HANASIF SECONDAR SCHOOL iliyopo kinondoni siku ya jumamosi tarehe 21/11/2015, na kuanza saa 2:00 hadi saa 9:30 na kutoka hapo ndipo tunaenda ukumbini wa kijiji mnamo saa 10:00 jioni kwa ajili ya tafrija inayofanywa na wazazi wangu na kumalizika saa 2:00 usiku.

WOTE MNAKARIBISHWA KARIBU SANA

NAMBA ZA SIMU: 0712-243060, 0719-105412

S. silali
Sili silali

Kielelezo 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika barua rasmi badala ya kadi ya mwaliko. Hata hivyo, barua aliyoandika haikufuata baadhi ya kanuni za uandishi wa barua rasmi.


## 2.4 Sehemu D: Maendeleo ya Kiswahili

### Swali la 10: Maendeleo ya Kiswahili

Swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili*, lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kuchambua juhudi zilizofanywa na Chama cha Kiswahili cha Afrika (CHAKA) ili kukuza na kueneza Kiswahili Barani Afrika. Mtahiniwa alitakiwa kueleza majukumu matano (5) ya Chama cha Kiswahili cha Afrika (CHAKA) katika juhudi zake za kukuza na kueneza Kiswahili. Swali lilikuwa na alama 10.

Watahiniwa wengi (72.3%) waliojibu swali hili walishindwa kueleza majukumu ya Chama cha Kiswahili

Afrika (CHAKA) katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili na hivyo kupata alama 0 hadi $2^1/_2$. Asilimia 17.2 waliojibu swali hili walipata alama za wastani ambazo ni alama 3 hadi 4. Aidha, asilimia 10.5 ndio pekee waliojibu vizuri na kuweza kupata alama za juu ambazo ni alama $04^1/_2$ hadi 10. Chati Na. 4 inafafanua ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 4: Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia**

Swali hili ni mojawapo ya maswali yaliyojibiwa vibaya na watahiniwa wengi. Baadhi ya watahiniwa hao hawakuelewa majukumu ya CHAKA badala yake walielezea shughuli mbalimbali zilizosababisha kukua kwa Kiswahili na watahiniwa wengine walieleza kuhusu kuenea kwa Kiswahili enzi za ukoloni kama vile elimu, dini, biashara, vyombo vya habari na vita kama inavyoonekana katika Kielelezo 10.1.


**Kielelezo 10.1**

10 Yafuatayo ni majukumu ya chama hiki katika ku
fanikisha azma hiyo.
Elimu- Ilisaidia kukua na kuenea kwa kiswahili
Barani Afrika kwa haraka zaidi wakoloni waliku
ja wakatufundisha kusoma na pia wali tuletea vi
tabu ilisaidia kwa kiasi kikubwa kukua na kuene
a kwa kiswahili Barani Afrika.
Dini. Walituletea dini nayopia ilichangia kuenea
kwa kiswahili Barani Afrika walikuwa wanatumi
a Lugha ya kiswahili makanisani, misikitini ata
kwa wale waliokosa elimu walijua kiswahili kwa
haraka zaidi kwa kupitia dini. Walileta vitabu
vyadini vilivyo andikwa kwa Lugha ya kiswahili
Biashara - Wafanya biashara iliwasaidia ku
jua kiswahili kwa haraka zaidi wakoloni
waliokuwa wanakuja kwa wafanya biashara
walikuwa wanakuja na kutumia Lugha ya
kiswahili iliwasaidia wafanya biashara kuju
a na kuelewa kiswahili kwa haraka zaidi Ba
rani Afrika.
Vyombo vya habari - Vilisaidia kuenesa au
kusambaza lugha ya kiswahili kwa haraka
zaidi kwa sababu habari walizokuwa wanazi
toa walikuwa wanatangaza kwa kiswahili. Pi
ahii ni sababu kubwa iliyosaidia kuenea kwa
kiswahili. Afaambao walikuwa hawajapata eli
mu walikuwa wanasikia. vyombo vya habari
vilisaidia kusambaza au kuenea kwa kiswahili
Barani Afrika.
Vita- Ilisaidia kuenea kwa kiswahili hapa nchini
wakati wakiwa wanapambana walikuwa wana
tumia lugha ya kiswahili - Afawale waliokuwa

Kielelezo 10.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza majukumu ya Chama cha Kiswahili Afrika (CHAKA) badala yake alielezea shughuli mbalimbali zilizosababisha kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi za ukoloni.

Hata hivyo, watahiniwa wachache sawa na asilimia 27.7 waliweza kueleza majukumu ya Chama cha Kiswahili cha Afrika (CHAKA) katika juhudi zake za kukuza na kueneza Kiswahili Barani Afrika. Kati yao, asilimia 17.5 ya watahiniwa hao waliweza kuelezea majukumu mawili ya Chama cha Kiswahili cha Afrika katika juhudi zake za kukuza na kueneza Kiswahili Barani Afrika kama vile uchapishaji wa vitabu kwa lugha ya Kiswahili na kuandaa kozi maalumu za ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa hao hawakuweza kufafanua vizuri majukumu na hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 10.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuelezea majukumu mawili ya Chama cha Kiswahili cha Afrika katika juhudi zake za kukuza na kueneza Kiswahili Barani Afrika.

**Kielelezo 10.2**


SWALI 10

Chama cha Kiswahili cha Afrika (CHAKA) ni miongoni mwa asasi/vyombo cha kisheria zilizopo mstari wa mbele katika kukikuza na kukieneza Kiswahili Barani Afrika. CHAKA kilianzishwa mnamo mwaka 1978. Chama hiki kilianzishwa kikiwa na madhumuni yafuatayo;

Kukuza na kukieneza Kiswahili barani Afrika. Kama ilivyo kwa kirefu chake, CHAKA kina jukumu la kukipanua Kiswahili kulingana na matumizi pia hata ongezeko la watumiaji. Hii imetokana na mifano mahususi iliyofanywa kukuza na kukieneza Kiswahili. mf. uchapishaji wa vitabu ya lugha kwa lugha ya Kiswahili, kuandaa kozi maalumu za ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Hivyo kusababisha Kiswahili kikapate weza kukua na kuenea barani Afrika.

Kielelezo 10.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeelezea majukumu mawili tu kati ya matano aliyotakiwa kuyaeleza.

Aidha, asilimia 10.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili waliweza kueleza kwa usahihi majukumu manne hadi matano ya Chama cha Kiswahili cha Afrika (CHAKA) katika juhudi zake za kukuza na kueneza Kiswahili Barani Afrika. Mtahiniwa mmoja alielezea majukumu hayo kuwa ni: *Kuanzishwa kwa vyama vya Kiswahili, kutoa semina za Kiswahili, uandishi wa vitabu vya maarifa na kufanya utafiti*. Watahiniwa waliojibu swali vizuri walipata alama 5 hadi 10. Kielelezo 10.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza majukumu ya *CHAKA kwa usahihi.*


**Kielelezo 10.3**

107 Chama cha kiswahili cha Afrika (CHAKA)
ni moja ya vyama vilivyoundwa ili kukuza
na kueneza kiswahili barani Afrika. CHAKA
ni chama kilicho undwa baada ya BAKITA
kuundwa. Chama hiki kimeweza kuwa na
manufaa mengi kwa vyama vingine na pia
kwa Afrika . Yafuatayo ni majukumu ya
chama hiki:-

Kuitisha na kuanzisha semina mbalimbali kuwa
ya lugha ya kiswahili:- Chama cha kiswahili
cha Afrika kimeweza kuitisha semina mbali
juu ya kukuza lugha ya kiswahili ili
kueneza matumizi sahihi ya lugha hiyo.
Hivyo hili ni moja ya majukumu mbalimbali
ya chama cha kiswahili Afrika katika kui
kuza na kueneza kiswahili Barani Afrika.

Uandishi na usambazaji wa majarida
mbalimbali yanayo husu lugha ya kiswahili.
Chama cha kiswahili Africa kimeandika na
kusambaza majarida mbalimbali yanayohu
su lugha ya kiswahili ndani na nje ya
nchi. Hii yote ni kuifanya lugha ya kiswa
hi kupanuka na kuweza kutumika hadi
nje ya nchi. Kwa kitendo hicho kili fanya lugha
ya kiswahili kukua na kuenea maeneo mbali
mbali nchini na hadi nje ya nchi.

Kuhamasisha na kusaidia watunzi wa kazi
za fasihi:- Chama cha kiswahili cha Afrika pia
kimesaidia watunzi wa kazi za fasihi kama
watunzi wa mashairi, riwaya na tamthiliya. Hi
vyo kufanya lugha kuweza kutumika kifasaha


10 Zaidi. Hii ni moja ya majukumu ya CHAKA katika kukuza na kueneza kiswahili Barani Afrika.

Kuhamasisha na kusaidia vyama vingine katika kukuza na kueneza kiswahili: CHAKA imeungana na vyama vingine ambavyo vipo katika kukuza na kueneza lugha ya kiswahili. CHAKA imesaidia na inasaidia vyama vingine ili kuweza kufikia lengo la kueneza lugha ya kiswahili ndani na nje ya nchi. Hivyo hii ni moja ya majukumu ya chaka katika kukuza na kueneza lugha Afrika.

Kuhamasisha juu ya matumizi sahihi ya lugha: Chama cha kiswahili cha Afrika kinaamasisha juu ya matumizi sahihi ya lugha. Kuhamasishwa kwa matumizi sahihi ya lugha imechangia sana katika kukuza na kueneza lugha Afrika.

Hitimisho: Vyama hivi vinakazi kubwa katika kulinda lugha yetu. Hivyo basi tuvisaidie na tuviunge mkono katika kazi hii.

Kielelezo 10.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza majukumu ya Chama cha Kiswahili cha Afrika (CHAKA) kwa usahihi.

## 2.5 Sehemu E: Fasihi kwa Ujumla

### 2.5.1 Swali la 11: Utungaji wa Kazi za Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Utungaji wa Kazi za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima maarifa katika kutunga kazi za fasihi. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua kwa mifano kanuni nne za utunzi wa mashairi ya kimapokeo na lilikuwa na alama 15.

Asilimia 62.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu kwa usahihi ambapo asilimia 35.1 walipata alama $7^1/_2$ hadi 14. Baadhi ya watahiniwa waliweza kufafanua kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo na kutoa mifano kama vile *uwepo wa urari wa vina na mizani, muundo wa beti na kituo ambacho hufafanua kila ubeti*. Aidha, watahiniwa wengine waliweza kuandika utangulizi mzuri, hitimisho lililokidhi matakwa ya swali na walibaini kuwa mashairi ya kimapokeo lazima yawe na ujumbe ndani yake. Kielelezo 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo kwa kutoa mifano maridhawa.

**Kielelezo 11.1**

11 Mashairi ya kimapokeo ni mashairi ambayo hufuata urari wa vina na mizani, haya hutofautiana na mashairi ya kisasa ambayo si lazima yawe na urari wa vina na mizani. Zifuatazo ni kanuni muhimu nne za utunzi wa mashairi ya kimapokeo


Mashairi ya kimapokeo lazima yawe na urari wa vina na mizani hii ni shera na kanuni ambayo mtunzi wa mashairi ya kimapokeo hufuata ambapo vina vya nusumstari vinatakiwa vifanane na hata vina vya mwishoni mwa mstari vinatakiwa vifanane pia.

Mashairi ya kimapokeo lazima yawe na muundo wa beti hii ni mkusanyiko wa mistari zaidi ya mmoja ya shairi ambayo beti huweza kuundwa na mistari minne, mitano, na hata zaidi ya hiyo kwa hiyo shairi la kimapokeo lazima liwe na muundo wa beti mfano

Nchi yangu Tanzania, Ardhi yako furahia
Kwa rutuba jivunia, Ndani na hata dunia
Nafasi kwanza chukua, Na hivyo usita kimbia
Jina lako na sifa, nazuri wa sofia

huo ni ubeti ambao unaundwa na mistari minne na wenye urari wa vina na mizani.

Mashairi ya kimapokeo huwa yana kituo ambacho hufanana kwa kila ubeti kituo ni mstari wa mwisho wa kila ubeti ambao hufanana kwa kila beti mstari huo huwa na maneno yanayotoa maana iliyoko kwenye shairi zima kwa ujumla, hivyo kituo ni lazima kiwepo katika shairi la kimapokeo



mfano: Nchi yangu Tanzania, Ardhi yako furahia
Kwa rutuba jiyunia ndani hata kwadunia
Nafasi kwanza chukua, na hivyo vita kimbia
Jino lako we ni sifa, na uzuri wa sophia
mstari wa mwisho huo ndio mstari unao wakilisha kituo ambacho hufanana kwa kila ubeti. Jino lako we ni sifa, na uzuri wa sofia".
Mashairi ya kimapokeo lazima yazungumzie Juu ya jambo fulani (yawe na ujumbe ndani yake) hii ni sawa na ni lazima mashairi yawe yanazungumzia Juu ya jambo fulani. mfano Juu ya gonjwa hatari la Ukimwi, Utumiaji wa madawa ya kulevya, katiba ya nchi, Ukoloni na hata utunzaji wa misitu.
hivyo basi Sheria tajwa hapo juu ni Sheria ambazo mtunzi wa shairi la kimapokeo anapaswa kufuata ili kukidhi na kuhakikisha utunzi mwema wa mashairi.

Kielelezo 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua vizuri kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo.

Aidha, asilimia 37.7 ya watahiniwa walishindwa kufafanua kwa kutoa mifano ya kanuni nne za utunzi wa mashairi ya kimapokeo na hivyo kupata alama 0 hadi 4. Miongoni mwao, asilimia 9.1% walipata alama 0. Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi, kwani walitumia vitabu teule vya fasihi andishi badala ya kufafanua kanuni nne zitokanazo na fasihi simulizi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia diwani ya *WASAKATONGE na MALENGA WAPYA* kufafanua dhamira mbalimbali zilizojitokeza katika diwani hizo badala ya kufafanua kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo. Kielelezo 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 11.2**

11 Kwa kutumia Mifano, kufafanua kauli ni muhimu nne (4) za Ultuzi kwa Mashairi ya kimapokeo.

Kwa kutumia diwani ya WASA KATONGE ambao Mwandishi ni MOHAMED SEIF KHATIBU na pia Kwa kutumia diwani ya MALENGA WAPYA ambao Mwandishi ni Taasisi ya Kiswahili na lugha za Kigeni ambao wamejadili mambo mbalimbali ambayo ni.

Kwa kuanzia na diwani ya WASAKATONGE ambayo Mwandishi ni M.S.Khatibu amejadili mambo ambayo yanahusiana na Vitu mbalimbali ambazo ni kafuatayo.

Usaliti na Unafiki, mwandishi anatuambia Kwamba Usaliti ni kikwazo ambacho kimekwaza jamii nyingi. ambao ni mfano wa shairi la "Wasodhabi" ambao anatuambia kwamba usaliti ni kikwazo kikubwa katika jamii.

Mmomonyoko wa Maadili, Mwandishi anatuambia Kwamba Kuna Maadili Mema ambayo yanayohusu Kuleta Maadili Mema. Mfano shairi la "tuyaziga tio haya" na "Jiwa si ndi"

Kupiga Vita Ukoloni Mamboleo, Mwandishi anatuambia Kwamba tupige Vita Ukoloni Mamboleo. Mwandishi amatuambia katika shairi "tuyazigatio haya"

pia Kwa kuanzia na ushairi wa ~~WASAKATONGE~~ MALENGA WAPYA ambao Mwandishi ni TAKILUKI ambayo Mwandishi amejadili Mambo Kafuatayo ambayo ni

Uongozi mbaya, Mwandishi anatuambia Kwamba kupige Vita ambapo pale serikali haitaki kutimiza haki yao mwandishi anatuambia katika shairi la "puuzo"


Maadili mema na Maonyo katika jamii, Mwandishi anatuambia Kwamba jamii yetu inapaswa kuwa na Maadi Mema katika jamii na Maonyo Mazuri katika jamii yetu yabo:

Kielelezo 11.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejikita katika kujadili dhamira kutoka katika diwani za *WASAKATONGE* na *MALENGA WAPYA*.

### 2.5.2 Swali la 12: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi*, *Uhakiki wa Ushairi* na lililenga kupima tathmini. Swali liliwataka watahiniwa kutumia hoja tatu kutoka katika kila diwani kati ya mbili walizosoma ili kuthibitisha kauli kuwa kazi za fasihi hufichua mivutano iliyopo katika jamii. Swali lilikuwa na alama 15.

Asilimia 59.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifanya vizuri. Miongoni mwao, asilimia 45 walipata alama za juu ambazo ni 7 hadi 15. Asilimia 14.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani ambazo ni $4^1/_2$ hadi $6^1/_2$. Aidha, asilimia 40.1 ya watahiniwa walipata alama chini ya wastani ambazo ni alama 0 hadi 4. Chati Na. 5 inafafanua ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.





**Chati Na. 5: Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia**

Watahiniwa waliojibu vizuri (45%) waliweza kutaja mivutano iliyopo katika jamii kama vile *mivutano ya kimatabaka, mivutano katika masuala ya kidini na mivutano katika matumizi mabaya ya madaraka.* Aidha**,** watahiniwa wengine *waliweza kutaja mivutano katika familia*, *mivutano inayohusu ukale na usasa* na *mivutano ya wananchi na ofisi za umma*. Kielelezo 12.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya

mtahiniwa aliyejibu swali kwa hoja tatu sahihi kwa kila kitabu kutoka katika vitabu teule viwili.

**Kielelezo 12.1**



12. Mivutano; Ni hali ya kutoelewana baina ya pande mbili. Mivutano hiyo yaweza kuwa ya Kijamii Kiutamaduni, Kisiasa na ya Kiuchumi. Kwa kutumia diwani mbili kati ya "Wasakatonge" kilichoandikwa na "Mhe Seif Khatibu" na diwani ya "Malenga wapya" kilichoandikwa na "Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni".

Kwa ujumla waandishi hawa wa diwani hizi wameonyesha mivutano hiyo kwa kutoa hoja m-balimbali.

Kwa kuanzia na diwani ya Wasakatonge - mwandishi amezungumzia suala la mvutano kwa kutoa hoja kama zifuatazo

12. Mivutano iliyopo Kati ya tabaka la juu na tabaka la chini; Katika diwani hii mwandishi ameonyesha mivutano hiyo Katika shairi la "Miamba" ambapo amesema:

"Miamba
Chui na Simba mbugani
Mbugani wanatamba
Majani hayaliki
Je ni sheria ya mbuga"

Mwandishi amewazungumzia chui na Simba akimaanisha ni tabaka la juu ambapo tabaka la chini haliwezi kula majani kutokana na unyonge wao Kwahiyo hivyo ameamua Kuonyesha mivutano hiyo

Mivutano iliyopo Katika masuala ya dini; Mwandishi ameonyesha mivutano iliyopo Katika masuala ya dini Katika shairi la "Uasi" ambapo mwandishi amesema:

"Uasi
Katika dini
Masheikh na Masharifu
Mapadri na Maaskofu
Kauli zao nadhifu
kujigamba ni waongofu
Wengi wao ni wachafu
dini wanazikashifu
Wanafiki."

mwandishi ameonyesha jambo ili kuwa si nzuri hivyo alihamua kulifichua

Mivutano iliyopo Kuhusu Unyanyasaji; Katika diwani hii mwandishi ameonyesha mivutano Kuhusu unyanyasaji Katika shairi la "Kosa" ambapo amesema:

12. "Mitunyanyase
Sio Watwana
Watu wamana
Tulungana
Kwa heshima na tahadhima"

hapa mwandishi ameamua afichue mivutano-hiyo iliyopo ndani ya jamii kuhusu unyanyasaji kutokana na umaskini.

Mivutano iliyopo kuhusu Uchu wa madaraka; Katika madaraka kuna mivutano mingi ambapo ~~ina~~ ameonyesha katika shairi la "Tonge la Ugali" ambapo amesema

" Wanapigana
Waumizana
Wauwana
Kwa tonge la Ugali"

Mwandishi ameonyesha ni jinsi gani mivutano inatokea katika jamii kwa kugombania madaraka ambapo inapelekea vifo kwa jamii hivyo ameamua kufichua.

Mivutano iliyopo kuhusu Udini na Ukabila katika jamii; Mwandishi hamefichua jambo hili katika shairi la Afrika ambapo amesema "Lini

Afrika utakuwa
bara lenye amani
Udini kufyeka
Ukabila kuzika
Ni lini"

hivyo basi mwandishi ameona jinsi Afrika inavyotengeneza kutokuwa na umoja ~~a~~ kupotia Udini na Ukabila na kuhamua kufichua jambo.

12. pia katika diwani ya Malenga wapya - mandishi amefichua ~~mamb~~ mivutano iliyopo kwa kutoa hoja mbalimbali

Mivutano iliyopo ni kuhusu ukoloni mamboleo; katika diwani hii mwandishi ameonyesha suala hili ambapo inaleta mivutano kama ya watu ~~ha~~ ambapo katika shairi la "Hali halisi" ambapo amesema:-

"Hali hii yashangaza, Nasi yatulemaza
Kimekuwa miujiza, Yapaa kujiuliza
Mshumaa unawaka, Giza linazidi"

hivyo basi kutokana na Msuguano mwandishi ameamua kufichua mivutano hii.

. Mivutano iliyopo kuhusu Uongozi mbaya; shairi la "Mpaka lini" ndipo mwandishi amefichua mivutano hiyo ambapo amesema:-

"Jamani ~~mb~~ mambo gani haya, Mnayotu fanyia
Tena bila ya huruma, Mnaturembea
Tumebaki ~~k~~ kwalalama, shida twajionea
Mpaka lini mtaturemea"

hapa mwandishi anaonyesha ~~mambo kambayo~~ kiongozi anayafanya pasipo kuthamini na kujali wananchi wake

Mivutano iliyopo ~~kuta~~ kuhusu Unyonyaji wa maliasili; katika shairi la Mpaka lini mwandishi amethibitisha kauli hii ambapo ~~a~~ amesema

"Msema kweli, kwenu ni chagizo
Mtakabihali, hauiki mbele ya vikwazo
Muongo sana, kwenu nyinyi ni kigezo
Mpaka lini mtaturuhezea!"

hivyo basi mwandishi ameonyesha ni jinsi gani jamii inayotawaliwa inadharauliwa kiasi ambacho si kizuri hivyo basi ameamua kufichua jambo hili.

Kwahiyo Waandishi wamejitahidi kufichua mivutano ambayo hipo miongoni mwa jamii kwa lengo la kuleta maelewano.

Kielelezo 12.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejadili mivutano kama ilivyofichuliwa na waandishi wa diwani mbili.

Aidha, asilimia 20.4 ya watahiniwa walipata alama za wastani ambazo ni $4^{1}/_{2}$ hadi $6^{1}/_{2}$ kwa kuwa baadhi yao waliweza kufichua mivutano iliyopo katika jamii kwa hoja moja tu au mbili kati ya tatu kutoka katika diwani teule mbili walizosoma. Pia wapo watahiniwa walioweza kuandika utangulizi mzuri, lakini wakaeleza hoja moja tu kutoka katika kitabu teule kimoja tu kuthibitisha kauli isemayo kuwa kazi za fasihi hufichua mivutano.

Hata hivyo, asilimia 40.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walishindwa kujibu swali kwa usahihi na hivyo kupata alama 0 hadi 4, kati yao asilimia 18.9 walipata alama 0. Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha utanzu wa ushairi na tanzu nyingine za fasihi andishi kwa sababu, baadhi ya watahiniwa hao walitumia vitabu vya Riwaya badala ya vile vya Ushairi na wengine walitumia vitabu vya Tamthiliya badala ya vitabu vya Ushairi kama swali lilivyoelekeza. Kielelezo 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetumia vitabu vya Riwaya badala ya vitabu vya Ushairi kinyume na maelekezo ya swali.

**Kielelezo 12.2**

12. Kazi za fasihi hufichua mivutano iliyopo katika jamii. Kwa kutumia hoja tatu kwa kila diwani fafanua mivutano hiyo kutoka katika diwani mbili ulizosoma.

JIBU.

Kazi za fasihi hufichua mivutano iliyopo katika jamii. Kwa kutumia hoja tatu kwa kila diwani nina fafanua mivutano hiyo kutoka katika diwani mbili nilizosoma kama ifuatavyo. na nitatumia diwani ya "WATOTO WA MAMANTILIE" na "TAKADINI".

Kwa kuanzia na diwani ya "WATOTO WA MAMANTILIE":

Katika diwani hii ya Watoto wa mamantilie mwandishi amejaribu kuonesha jinsi kazi za fasihi hufichua mivutano iliyopo katika jamii kama ifuatavyo.

Kwanza tunaona mvutano uliojitokeza katika diwani hii kwa Mhusika Mamantilie na Mumewe Mzee Lomolomo. Wahusika hawa walikuwa na mvutano kwasababu Mzee lomolomo alikuwa hashughulikii familia yake kwa hudu ma yeyote ile na akawa amejiunga katika kundi la Ulevi na [illegible] kila anacho kipata yeye anakitafunia ulevi.

Pia tunaona mvutano wa Mwalimu chikoya na watoto wa mamantilie jinsi walipokuwa shuleni na mvutano huwo ulijitokeza wakati Mwalim chikoya alipowafukuza watoto wa Mamantilie skuli kwa sababu hawakulipa ada za shule na pia walikuwa hawana sareza skuli.

Vilevile ~~[illegible]~~ mvutano mwengine ulijitokeza wakati Mamantilie alipokuwa akimkataza mumewe ambaye ni Mzee Lomolomo kuachana na ulevi ili yeye aliku hamskilizi mmke wake alikuwa anafanya anavyo taka yeye tu.

Hivyo Kazi za fasihi zimefichua ~~[illegible]~~ mivutano ilipo katika jamii.

Kielelezo 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetumia vitabu vya Riwaya badala ya vitabu vya Ushairi kinyume kabisa na matakwa ya swali husika.

### 2.5.3 Swali la 13: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi*, *Uhakiki wa Riwaya*. Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kufanya tathmini na lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha hoja isemayo:- *Mandhari ikiteuliwa vizuri humsaidia sana mwandishi katika kufikisha yale aliyokusudia kwa jamii yake.* Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja tatu kutoka katika kila kitabu na lilikuwa na jumla ya alama 15.

Asilimia 53.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walishindwa kujibu vizuri kutokana na kutoweza kubaini ni kwa jinsi gani mandhari iliyoteuliwa vizuri inaweza kumsaidia mwandishi katika kufikisha ujumbe kwa waliokusudiwa. Watahiniwa hao walipata alama 0 hadi 4. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 23.8 walipata alama 0 kwa sababu baadhi yao walijikita katika kueleza wasifu wa wahusika katika vitabu teule badala ya kuwatumia wahusika kuonesha mahali walipofanyia matukio mbambali ambayo kwa kufanya hivyo wangekuwa wameonesha mandhari ilivyomsaidia mwandishi kutoa ujumbe aliokusudia kwa jamii husika. Aidha, wapo watahiniwa walioeleza migogoro iliyojitokeza ndani ya vitabu teule kama ile ya familia ya Mzee Lomolomo katika riwaya ya *WATOTO WA MAMA N'TILIE* jambo ambalo halihusiani na mandhari iliyotumika. Kielelezo 13.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali kwa kuelezea wasifu wa wahusika na migogoro.


**Kielelezo 13.1**

B. Kudhibitisha hoja hiyo kwa kutoa mfano
mifano toka katika kitabu kati ya
riwaya mbili zilizoorodheshwa.
watoto wa mamantilie E. mbogo (HP)
mwaka 2002.
mamantilie aliweza kuwa somesha watoto wake baadaye aliwashindwa pale mzee lomolomo kwenda kilabuni kila siku kunywa pombe
watoto wa mamantilie
- ni mama nyenye huruma
- ni mama nyenye busara
- ni mchapakazi
- anafaa kuigwa katika jamii
- ni mama nyenye msimamo
- ni mama wa suzi

mzee lomolomo
- Hafai kuigwa
- ni baba nyenye kuibisha jamii
- ni mzee mlevi
- hana heshima

peter na doto
ni pale peter na doto kukutana kwenye dampo ya takataka na kupigana kwa sababu ya mnozo iliyokuwenye dampo zaina aliweza kushauri peter kwamba mwache jirani yako doto

suzi
- ni mtoto wa mamantilie
- ni mtoto mwenye heshima
- ni mchapakazi


anafaa kuigwa
zainabu
Ni mtoto wa mzee lomolomo.
mzee lomolomo ana wake wawili
hafai kuigwa katika jamii pale
mamantilie kuuza mandazi mitaa
ni na mjijini mzee lomolomo hataki
ni kutokana na ubunifu wa mama
ntilie
zita
- ni dada yake na peter
- ni mtoto wa mzee lomolomo
- ni msichana mwenye huruma
- pale doto kupigwa na peter ali
msaidia sana
- anamahusiano ya kimapenzi na
doto
- peter na doto alipigana kweny
e dampo ya takataka kwasaba
bu ya mmoto
migogoro iliyojitokeza ni pale
migagoro baina ya peter na doto.
ni pale peter kulopenda doto kweny
e dampo ya takataka.
migagoro baina ya mamantilie
na mzee lomolomo: ni pale mzee
lomolomo akikewa analukama mama
ntiele na kupigwa na mzee lomolom
o
migogoro baina ya zita na zaina
bu ni pale anapoolewa na doto
zita zainabu anatakuvunanja

Kielelezo 13.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeelezea wasifu wa wahusika na migogoro tofauti na matakwa ya swali.

Hata hivyo, asilimia 14.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama $4^1/_2$ hadi $6^1/_2$ ambazo ni ufaulu wa wastani. Aidha, asilimia 26.9 walifanya vizuri zaidi na kupata alama 7 hadi 15, kwa sababu baadhi yao waliweza kutumia mandhari kueleza matabaka yalivyojitokeza katika jamii, umaskini na hali duni ya maisha na watahiniwa wengine waliweza kuzitaja hoja na kuzifafanua ipasavyo ili kuonesha namna mwandishi anavyoweza kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa kutumia mandhari. Kielelezo 13.2

kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye aliweza kuthibitisha hoja ya uteuzi wa mandhari katika kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa.

**Kielelezo 13.2**

13 Mandhari ni sehemu ambayo mwandishi huonesha kazi yake ya fasihi kuendana na mazingira hayo. Katika riwaya ya "Takadini" iliyoandikwa na "Ben J. Hanson na riwaya ya "Watoto Wa Mamantilie" waandishi wameweza kufikisha yale yaliyokusudiwa kwa jamii yake. Kwa kuanza na riwaya ya "Takadini" mwandishi ameonesha kama ifuatavyo.

Mwandishi ametumia madhari ya dampo. Mwandishi anaelezea kwamba bado wapo watu wanaoishi katika lindi la umaskini kama Peter, Kurwa na Doto mpaka wakawa wanaenda kutafuta chakula kwenye dampo suala hili linaashiria wazi juu ya umaskini

13. Madhari ni sehemu ambayo mwandishi hufikisha ujumbe kuendana na mazingira. Katika riwaya ya "Takadini" iliyoandikwa na mwandishi "Ben J. Hanson" na riwaya ya "Watoto Wa Mamantilie" iliyoandikwa na "E. Mbogo" wameweza kuonesha mambo yaliyoko kwenye Jamii kuendana na madhari. Kwa kuanza na riwaya ya "Takadini" mwandishi ameonesha

Mandhari ya msituni. Hii inaashiria wazi pale ambapo Sekai alipoamua kutoroka na mwanae ili kuokoa maisha yake na Takadini mwandishi ameweza kuliweka suala hili katika jamii kwani, kutokana na dhana potofu Sekai aliamua kutoroka.

Mandhari ya kijijini. Hii inaelezea wazi kwamba mandhari iliyotumika ni ya

13 kijijini ambapo walikuwa wanaamini kwamba walemavu hawapaswi kuishi na kusababisha maafikino kuwana mwandishi anafikisha ujumbe kwamba kwani hata hao wanayo haki ya kuishi.

Mandhari ya mtoni. Hapa anaonesha Shingai alivyodamya kumsaidia kuchota maji nyumbani kwa Sekai na hatimaye kupelekea ugomvi kwani wazazi wake waliamini kwamba Shingai anatakiwa kuolewa na Mhamo na walikuamini kwamba Shingai anayo mahusiano na Takadini na kupelekea kuwa na ugomvi kwani si vizuri kumchagulia mtu mume.

Hata hivyo katika riwaya ya "Watoto Wa Mamantiliye" ameonesha mandhari kama ifuatavyo.

Mandhari ya dampo. Mwandishi anaelezea kwamba bado wapo watu wanaoishi katika limbuko la umaskini kama Peter, Zita, Kurwa na Doto na kuwapelekea kwenda kutafuta chakula dampo. Suala hili linaashiria bado suala la umaskini limetawala katika jamii nyingi.

Mandhari ya shuleni. Mwandishi ametumia mandhari hii kwani watoto hawakuwa na elimu kama akina Musa, Peter, Zita kwasababu ya kukosa ada na hela ya sare na kupelekea kufukuzwa shule. Serekali inapaswa iweke mkazo kwa kuwasaidia sare na ada kwa wasio na uwezo.

Mandhari ya mjini. Ameweka wazi mandhari ya mjini kwani bado wapo watu kama akina mamantiliye wanaonyanyaswa na kunyimwa haki zao za msingi kwani bado

13. hawathaminiwi na wamebaki kuhangaika huko mjini. Jamii inapaswa iwasaidie kwa kuwapa mikopo na elimu ya biashara.
Mandhari imeweza kufikisha ujumbe katika jamii na kuyaweka wazi mambo ambayo ni vizuri yapingwe kuendana na jamii ya sasa.

Kielelezo 13.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye aliweza kutoa hoja zinazoafiki kwamba uteuzi mzuri wa mandhari ni muhimu katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii.

### 2.5.4 Swali la 14: Uhakiki wa Tamthiliya


Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi*, *Uhakiki wa Tamthiliya*. Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kufanya uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze jinsi waandishi walivyoonesha athari za utamaduni wa kigeni katika maadili ya jamii ya Kiafrika. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15.

Asilimia 54.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 4. Miongoni mwao, asilimia 14.2 walipata alama 0 kwa sababu walishindwa kuelezea jinsi waandishi walivyoonesha athari za utamaduni wa kigeni katika maadili ya jamii ya Kiafrika, kama vile uhusiano na ndoa, utandawazi, utumiaji wa madawa ya kulevya na maadili. Aidha, wapo watahiniwa walioelezea dhamira mbalimbali kwa kutumia kitabu teule cha Ushairi badala ya kitabu teule cha Tamthiliya kama swali lilivyoelekeza. Majibu haya ambayo sio sahihi yanaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa hawana maarifa ya kutofautisha vitabu teule vya fasihi andishi (Riwaya, Tamthiliya na Ushairi) Kielelezo 14.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejadili dhamira kwa kutumia kitabu teule cha Ushairi badala ya kile cha Tamthiliya.

**Kilelezo.14.1**

14 Kwa kutumia tamthilia mbili miongoni mwa zilizoorodheshwa kueleza
jinsi waandishi walivyoonyesha athari za utamaduni wa kigeni katika
maadili ya jamii ya Kiafrika.

Nalenda kutumia tamthilia mbili miongoni mwa zilizoorodheshwa ambazo
ni Malenga wapya na wasakatonge kwa kuanza na malenga wapya.
Malenga wapya ni tamthilia inayoeleza masuala mbalimbali katika
jamii. Kama vile ukombozi wa mwanamke, umuhimu wa kilimo, matumi-
zi mazuri ya pesa, umuhimu wa kutatua matatizo katika jamii, umuhimu
wa kutenda mema, na athari za ukoloni mamboleo.
Maudhui
Dhamira kuu: Ukombozi
Katika diwani hii msanii amejadili dhamira ya ukombozi wa kiuchumi,
kisiasa, kiutamaduni na kifikra.
Ukombozi wa kiuchumi, katika kujadili ukombozi wa kiuchumi
msanii amesisitiza mambo muhimu yafuatayo. Kwanza, umuhimu wa uchumi (kuinua)
wetu. Katika suala la kuinua uchumi wa nchi yetu wasanii wanasema
kuwa kuna umuhimu wa kujenga uchumi imara ili kujenga taifa lenye
uwezo wa kujitegemea kiuchumi.
Katika shairi la "Tuzingatie haya" (uk 27-28) ~~Wasanii~~ Wasanii wana
sisitiza umuhimu wa kufufua uchumi wa nchi. Pia ili tufufue uchumi
wa nchi ni lazima tupunguze maneno na tufanye kazi kwa bidii pasipo
na ulegezi, wananchi wote tuungane na kuhamasishana (ubeti wa 2)
Pia na viongozi sote tufanye kazi kwa bidii (ubet 3). Tuondoe tofauti
zetu na tuelewane na tamaa ya utajiri. Beti za (2 na 4) zinasema
~~Tutime jama~~ tulime, ~~tusitin~~
2. Uchumi kufufua, si hotuba ndefu sana
Moja litasaidia, ni kuhamasishana
Jingine litalofuatia, sote kushirikiana
Tuyazingatie haya, wala tusirudi nyuma.



14

4. Tufanye kazi lazima, tuache utegezi
Na jingine la kukoma, kuweko kwa uchegezi
Kutuletea lawama, ni mambo ya kihuni
Tuyazingatie haya, wala tusirudi nyuma.

Ukombozi wa kiutamaduni; katika ukombozi wa kiutamaduni mshairi amezungumzia juu ya ukombozi wa mwanamke. Ukombozi wa mwanamke ni jambo la msingi na la umuhimu katika jamii. Mwanamke akikombolewa ni sawa na jamii nzima kukombolewa, shairi la 10 "Kifungo" mwandishi anasema.

7. Kwa kuwa ni mwanamke, ndani mnanifinika
Lazima nije nitoke, kufata mengi fika
Nimechoshwa na ufukara, sitaki kudhalilika.
Kifungo kimenichosha, minyororo nimefungwa

Ili aweze kujitegemea mwenyewe, mwanamke anahitaji kuwa huru, na siyo kufungwa fungwa ndani na kumtegemea mume.

Ukombozi wa kisiasa katika "Samaki mtungini" Lukiraduka 19 kinaonyesha harakati za watu wa tabaka la chini kuondokana na utumwa wa kutawaliwa na kugandamizwa na wakoloni. Samaki anawakilisha watu wa tabaka la chini na mtungi anawakilisha mtawala ambao ni wakoloni au tabaka tawala.

Ukombozi wa kifikra, katika shairi la "Usiwe Bendera" uk 31 limezungumzia juu ya ukombozi wa kifikra au kimawazo. Jamii inahamasishwa isiwe bendera kufuata uelekeo wa upepo bali ijitegemee kimawazo.

Kielelezo 14.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejadili dhamira kwa kutumia kitabu cha Ushairi badala ya Tamthiliya.

Asilimia 45.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama $4^1/_2$ hadi 15, ambapo miongoni mwao, asilimia 27.4 walipata alama $4^1/_2$ hadi $6^1/_2$ ambazo ni alama za wastani kwa kuwa waliweza kutaja athari za utamaduni wa kigeni katika maadili ya jamii ya Kiafrika na kushindwa kufafanua ipasavyo.

Aidha, asilimia 18 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 7 hadi 15, kwa vile baadhi yao waliweza kuzitaja tamaduni hizo kama vile *watoto kwenda katika*

*kumbi za starehe, mapenzi katika umri mdogo na matumizi ya madawa ya kulevya*. Kielelezo 14.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye aliweza kuelezea jinsi waandishi walivyoonesha athari za utamaduni wa kigeni katika maadili ya jamii ya Kiafrika kwa usahihi.

**Kielelezo 14.2**

14. Utamaduni ni hali au maisha ya jamii
fulani katika maisha yake ya kila siku wana
yoishi. Ni kweli kwamba waandishi wamewe
za kuonesha athali za utamaduni wa kigeni
ambao umeweza kuharibu maadili ya jamii ya
Kiafrika kwa mfano Uvaaji, mawasiliano na
hata lugha kwa kutumia tamthiliya ya "ORODHA
iliyo andikwa na mwandishi Steve Reynolds
pamoja na tamthiliya ya "KILIO CHETU" iliyo
andikwa na mwandishi Medical Aid Founda
kwa kutumia tamthiliya ya Orodha.
kumbi za starehe pamoja na baa. katika tam
thiliya hii ya Orodha mwandishi ameweza
kuonyesha jinsi tamaduni za kigeni zilivyo hari-
bu maadili ya jamii za kiafrika kwa mfano
Furaha pamoja na rafiki yake Mary wanatoroka
nyumbani na kwenda baa mahali ambapo
ni hatarishi kwa sababu mambo mengi maovu
huweza kutokea na pia tukiangalia katika
tamaduni zetu za nyuma baa hazikuwepo
lakini kulikuwa na mkusanyiko ambapo watu
wazima kusanyika katika eneo moja kwa ajili ya
kufurahia kama vile kucheza ngoma na kui-
mba nyimbo za utamaduni vitu ambavyo
haviwezi kufanyika baa hata kumbi za starehe
lakini baada ya wageni kuleta tamaduni
hii ambayo ni asili yao wameweza kuharibu
maadili ya jamii ya kiafrika.
Utumiaji wa madawa ya kulevya. mwandishi
ameweza kuonyesha jinsi jambo hili lilivyoweza
kuharibu maadili na tamaduni za kiafrika
kwa sababu vitu kama hivi vimeletwa na

14 tamaduni za kigeni ambapo chanzo chakeni tamaduni za huko nje hii maweza kudhihirika pale ambapo kitunda alipokuwa akijaribu kumshawishi furaha kutumia madawa ya kulevya jambo ambalo lingeweza kumuharibu furaha hata hivyo tabia hii imeharibu vijana wengi wa kiafrika na kupelekea walifanya vitendo vya aibu vinavyo enda kinyume na maadili ya kiafrika.

Uigaji wa tamaduni za kigeni. Hii nayo pia imeweza kuchangia athari na kuharibu maadili ya jamii ya kiafrika hii inadhihirika pale mhusika Furaha pamoja na Mary mavazi ambayo walikua wakivaa wakati wakiwa wanaenda baa ni mavazi ambayo hayapo katika maadili ya jamii za kiafrika na yameweza kuharibu jamii zetu.

Kwa kutumia tamthiliya "Kilio Chetu".

Picha na sinema za ngono. katika tamthiliya hii mwandishi ameweza kuonyesha jinsi maadili ya kiafrika yalivyoweza kuathiriwa na tamaduni za kigeni hii inaonyesha dhahiri pale ambapo Chogo, Joti pamoja na Mwarami walikua wakienda katika vibanda vya picha kuangalia picha za ngono vitu ambavyo si vizuri kwa maadili ya kiafrika na pia huweza kuleta hasara kutokana kwamba huongeza uchochezi wa mwili kwa matamanio ya kufanya ngono kwa mfano pale Mwarami alipokuwa akijaribu kumshawishi Anna ili afanye nae mapenzi kama alivyokuwa ameta zama katika runinga

| | |
|---|---|
| 14 | Mapenzi katika Umri mdogo. Hii nayo pia ni tamaduni ambayo imeletwa na wageni ambapo watoto wamekua wakijiingiza katika mapenzi wakiwa na Umri mdogo hii ni kutokana na vitu ambavyo wanaviona katika tamaduni za nchi nyingine jambo ambalo kwa maadili ya kiafrika siyo sawa lakini kwa wenzetu ni jambo la kawaida hii imeweza kuonekana kati ya Joti na Suzi ambao walikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwisho wa siku Joti akapoteza maisha kwa Ukimwi na Suzi kupata mimba pamoja na Ukimwi. |
| | Matumizi ya kondomu. Haya nayo yameweza kuharibu maadili ya kiafrika kwani watu wamekua wakitumia kondomu kwa kufanya ngono ovyo na pasipo Umri wa kuruhusu kufanya tendo hilo kitu ambacho kimeweza pia kuchangia kuharibu maadili ya kiafrika ambapo kwa maadili ya kiafrika anayeruhusiwa kufanya tendo la ndoa ni mtu aliyeoa au kuolewa lakini hilo limekuwa halifuatwi kutokana na tamaduni za kigeni kuathiri maadili ya kiafrika. |
| | Mwandishi amefanikiwa kuonyesha athari hizo kwani zimekuwa kwa hali halisi zikionekana katika maisha yetu ya kila siku kwa jamii inayotuzunguka hivyo inapaswa watu wachunguzwe kuwa tamaduni za kigeni siyo nzuri kwani zinaleta athari kubwa kwa jamii yetu hasa kwa vijana waliokumbwa na swala hili la utandawazi. |


Kielelezo 14.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza kwa usahihi athari za utamaduni wa kigeni katika maadili ya jamii ya Kiafrika.

### 2.5.5 Swali la 15: Utungaji wa Kazi za Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na lililenga kupima uwezo wa watahiniwa katika kuunda mawazo na liliwataka watahiniwa kueleza maana ya vigano na kisha

watunge vigano kwa kutumia methali isemayo, *Umdhaniaye siye kumbe ndiye*. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilikuwa ni la lazima, hivyo watahiniwa wote walilijibu. Asilimia 63.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 4. Asilimia 12.0 walikuwa na ufaulu wa wastani na kupata alama $04^1/_2$ hadi $6^1/_2$. Aidha, asilimia 24.8 walipata alama 7 hadi 15 hivyo kuwa na ufaulu mzuri. Chati Na. 6 inafafanua ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 6: Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia**

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya na watahiniwa wengi (63.2%). Miongoni mwao, asilimia 47.3 walipata alama 0. Watahiniwa hao, walishindwa kubaini maana ya vigano na kanuni za utunzi wa vigano. Baadhi ya watahiniwa hao, walibuni mada tofauti na ile waliyopewa katika swali na kuandikia vigano. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia mada ya *KATIBA YA TANZANIA* badala ya methali isemayo Umdhaniaye siye kumbe ndiye*!* Pia katika majibu yake alitunga shairi badala ya kigano. Kielelezo 15.1

kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetunga shairi badala ya kigano.

**Kielelezo 15.1**


15 (a) Vigano ni maneno yanayotamkwa yenye fikra sahihi na kutokuwa na ukweli wa jambo ndani ya ukweli

(b) Kutunga vigano tumia Methali

KATIBA YA TANZANIA

Ndugu zangu ekewani, Watu kutesekea pia
Kuzunguka kila buni, Kuambatia kuti 'a
tukiwe kikakini, Nchini yetu Tanzania
Nchi yetu tajiri sana, nchini yetu Tanzania

Ndugu tusimamema, Kutetea haki muhimu
Shelia kuzikimama, nchini katiba muhimu
Watu kutengatiga kama, Jamaki kwenyi kisimu
Nchi yetu tajiri sana, nchini yetu Tanzania

Serikali kwa Mwananchi, Tuyaonehaya jambo
Kwetu iwi ni nchi-wachi, Si muhimu jambo
Tushika yetu siri nchi, Wetu hakika jambo
Nchi yetu tajiri sana, nchini yetu Tanzania

Tusifiche ukwelini, nchini yetu tajiri sana
Tusivaye abu kalani, mikuyetu jambo sana
Miza yetu kwa kalani, heshima kusimama sana
Nchi yetu tajiri sana, Nchini yetu Tanzania

Kielelezo 15.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye ametunga shairi kuhusu Katiba ya Tanzania badala ya kuandika kigano.

Aidha, watahiniwa wachache (36.8%) kati ya watahiniwa waliojibu swali hili, walipata alama 7 hadi 15. Baadhi ya watahiniwa hao waliweza kutoa maana sahihi ya vigano na kuweza kutunga kigano kwa kutumia methali isemayo *Umdhaniaye siye kumbe ndiye*. Aidha, watahiniwa wengine walizingatia vipengele vya fani na maudhui katika vigano walivyotunga.

Kielelezo 15.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alitunga kigano chenye fani na maudhui

yanayokidhi ujumbe unaopatikana katika methali isemayo *Umdhaniaye siye kumbe ndiye.*

**Kielelezo.15.2**

15 (a) Vigano - ni hadithi fupi zinazobeba maonyo na zilizosheheni methali na misemo ili kuonya jamii.

15 b) UMDHANIAYE SIYE KUMBE NDIYE

Mzee Majuto pamoja na mkewe Sikujua walikuwa wamebarikiwa kupata mali nyingi na uwezo wao kiuchumi ulikua juu. Wazee hawa walikuwa na mtoto wao mmoja aliyeitwa Tabu. Walimlea mtoto wao maisha ya kitajiri hadi Tabu akawa hajui shida kwani chochote alichotaka alikipata, pia wazazi wake walimzoesha mtoto wao kwa kumpa hela za kuchezea ovyo.

Kama waswahili wasemavyo "hakuna marefu yasiyokuwa na ncha" hatimaye mzee majuto alifariki dunia. mkewe bi Sikujua aliendelea kumzoea mtoto wao vibaya kwani mali aliziacha ~~mke~~ mumewe bado zilikuwepo. "Bandu bandu humaliza gogo". Hatimaye mali zile zilikwisha kwani Bi Sikujua hakuwa anaendeleza miradi aliyoiacha mumewe "Hayawi ~~yaka~~ hayawi yakawa." Atimaye maisha ya bi Sikujua na mwanaye Tabu yakabadilika kuda ikawa ya shida na zile fedha Tabu alizozoea kupewa kukawa hakuna tena.

Kama waswahili wasemavyo "mazoea ni kilema" Tabu aliyezoea kuchezea fedha akaanza kupata shida kwanza alianza kuomba omba kwa watu na baada ya watu kumshtukia wakawa hawampi tena fedha. Ndipo tabu alipoanza kuwa na mkono mrefu. Waha-

15(b) ga walisema "mtu hanyimwi maneno bali tonge la ugali"! Watu wema wakampelekea
Bi Majuto taarifa za tabia ya Tabu mwanaye. Yeye akaja juu "Oh mwanangu si
mwizi... mnazingizia wivu wenu tu."

"Lisemwalo lipo kama halipo laja, bahati mbaye yaliyokuwa yakisemwa na watu juu ya tabia ya Tabu yalikuja kweli siku moja alienda kuiba dukani kwa mzee mmoja na huyo mzee alikuwa amekaa chonjo akimvizia. Hivyo baada ya Tabu kuchukua pesa tu na kuanza kukimbia ndipo kelele za mwizi...!! mwizi...!! zilisikika. Bi Sikujua naye bila kujua ni nani mwizi alikwenda mbio kushuhudia. Kutahamaki ni mwanaye Tabu amedakwa kuwa ndiye mwizi!! Bi Sikujua tena alizama mwanaye kwa huruma wakati akichukuliwa kupelekwa jela akajisemea mwenyewe laiti ningejua kwani "Umdhaniaye siye kumbe ndiye"!!.

Kielelezo 15.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alitoa maana sahihi ya vigano na kutunga kigano kizuri kwa kuzingatia vipengele anuwai vya fani na maudhui.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA

Ufaulu katika mada zilizotahiniwa mwaka 2015 ulikuwa mzuri ambapo asilimia **77.63** ya watahiniwa walipata wastani wa alama 30 na zaidi. Ufaulu huu umekuwa na ongezeko la asilimia**7.97** ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2014 ambapo wastani wa ufaulu ulikuwa **69.66**.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali katika mtihani wa Kiswahili unaonesha kuwa watahiniwa walifanya vizuri zaidi katika mada ya *Uandishi, Ufahamu na Ufupisho, Fasihi Simulizi na Uhakiki wa Fasihi Andishi katika Ushairi, Matumizi ya Lugha*, *Uhakiki wa Fasihi katika Riwaya* na *Uhakiki wa Fasihi katika Tamthiliya*

Mada ya *Ufahamu na Ufupisho* ambayo kwa mwaka 2014 wastani wa ufaulu ulikuwa asilimia 53.9 imekuwa na ongezeko la asilimia 34.6 kwa mwaka 2015 na kuifanya mada hii kuwa na ufaulu wa asilimia 88.5. Aidha, mada ya *Uhakiki wa Fasihi Andishi* - *Ushairi* ambayo ilikuwa na ufaulu hafifu (24.1%) kwa mwaka 2014 imekuwa na ongezeko la asilimia 35.8 na kuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa na asilimia 59.9. Mada ambazo zimebakia kuwa na wastani wa ufaulu mzuri ijapokuwa umeshuka ni *Uhakiki wa Fasihi Riwaya*, *Uhakiki wa Fasihi – Tamthiliya* na *Matumizi ya Lugha*.

Mada zenye ufaulu wa wastani ni pamoja na *Matumizi ya Sarufi* na *Utungaji wa Kazi za Kifasihi*. Aidha, mada ya *Maendeleo ya Kiswahil*i ilikuwa na ufaulu hafifu kati ya mada zote zilizotahiniwa.

Mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* haikujibiwa vizuri kwa sababu, watahiniwa hawakuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha kuhusiana na mada hiyo. Aidha, watahiniwa wengi wamekuwa na tatizo la kutozingatia kwa kina maswala yanayohusiana na Historia ya Lugha ya Kiswahili. Watahiniwa hao walikosa ujuzi na maarifa kuhusu vyombo mbalimbali vilivyoundwa kwa lengo la kukuza Kiswahili Barani Afrika hususani Chama cha Kiswahili cha Afrika (CHAKA).

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla Mtihani wa Kidato cha Nne katika somo la Kiswahili mwaka 2015 ulizingatia Muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalihusisha ngazi zote za majazi ya utambuzi yaani maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa kilikuwa ni kizuri ambapo wastani wa ufaulu kwa somo hili ni asilimia **77.63**

Uchambuzi huu unaonesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa kama vile kutofuata maelekezo ya swali, uelewa mdogo wa mada mbalimbali na hasa mada za *Sarufi* na *Utungaji wa Kazi za Fasihi*. Ili kuinua zaidi kiwango cha ufaulu kwa mada zote katika mtihani wa Kidato cha Nne, jitihada zaidi zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji katika mada ya *Sarufi* ili kuwajengea wanafunzi ujuzi wa kujieleza kwa ufasaha hasa ikizingatiwa kuwa Sarufi ndiyo msingi wa lugha. Aidha, kuhusu mada ya *Utungaji wa Kazi za Kifasihi* zinahitajika jitihada za makusudi ili kuwajengea wanafunzi ujuzi wa kuweza kutunga kazi mbalimbali za kifasihi ambazo hatimaye zitaleta tija katika kuwapata watunzi wa kazi za fasihi

Ufaulu huu unaonesha kuwa, zipo mada zinazohitaji kutiliwa mkazo katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* inaonekana kuwa na tatizo kubwa zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji kwani wastani wa ufaulu wa mada hii umeshuka kwa asilimia 6.2 kutoka asilimia 33.9 kwa mwaka 2014 hadi ufaulu hafifu (27.7%) kwa mwaka 2015.

Hata hivyo, jitihada zaidi zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada za *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali*, *Uhakiki wa Fasihi katika Riwaya* na *Uhakiki wa Fasihi katika Tamthiliya* ili kuongeza kiwango cha ufaulu kuwa kizuri zaidi katika somo hili. Aidha, walimu na wanafunzi wasisitizwe kutumia sarufi sahihi ya Kiswahili ili kujijengea weledi katika mada ya *Matumizi ya Sarufi* ili kuondokana na tatizo la kisarufi na la kimatumizi katika kutumia lugha ya Kiswahili. Kuhusu mada ya *Utungaji wa Kazi za Kifasihi* zinahitajika jitihada za makusudi ili kuwajengea wanafunzi ujuzi wa kuweza kutunga kazi mbalimbali za kifasihi ambazo hatimaye zitaleta tija katika kupata watunzi wa kazi za fasihi. Ni muhimu pia wanafunzi wahamasishwe kujifunza mada ya

*Maendeleo ya Kiswahili* hasa kwa kufanya mazoezi mbalimbali yanayohusiana na Historia ya Lugha ya Kiswahili

Mwisho, taarifa hii ya uchambuzi kuhusu majibu ya watahiniwa itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili na kutoa changamoto kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Hali hii itawafanya walimu na wanafunzi kuyaelewa makosa mbalimbali yanayosababisha ufaulu kutokuwa mzuri ili kuweza kufanya marekebisho kwa ajili ya kuinua kiwango cha ufaulu kwa miaka ijayo.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili inapendekezwa kuwa:

(a) Walimu waweke mkazo katika ufundishaji/ujifunzaji wa mada zote na hasa mada za *Sarufi, Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali na Utungaji wa Kazi za Fasihi.*

(b) Wanafunzi wasisitizwe kusoma vitabu teule vya Ushairi, Tamthiliya na Riwaya ili wapate maarifa ya kutosha kuhusu vitabu hivyo, pia walimu waweke mkazo katika ufundishaji wa vipengele vya fani na maudhui.

(c) Wanafunzi wahamasishwe kujihusisha na utunzi wa kazi za Fasihi hususan mashairi ya kimapokeo na vipera vya Fasihi Simulizi. Aidha, walimu watoe mazoezi mengi kuhusu nyanja hizo na kutoa mrejesho kwa wanafunzi.

(d) Wanafunzi wahimizwe kufanya mazoezi mengi kutoka katika mada zote ili kuwajengea ujuzi na weledi wa kuzielewa ipasavyo mada mbalimbali.

**KIAMBATANISHO A**

## UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALI MBALI

### 021 Kiswahili

| S/N | Mada | 2014 | | | 2015 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya maswali | Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Alama 30 au Zaidi | Maoni | Idadi ya maswali | Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Alama 30 au Zaidi | Maoni |
| 1 | Uandishi | 2 | 86.7 | Vizuri | 2 | 92.1 | Vizuri |
| 2 | Ufahamu na Ufupisho | 2 | 53.9 | Vizuri | 2 | 88.5 | Vizuri |
| 3 | Fasihi Simulizi | 1 | 66.3 | Vizuri | 1 | 62.3 | Vizuri |
| 4 | Uhakikiwa wa Fasihi Andishi - Ushairi | 1 | 24.1 | Hafifu | 1 | 59.9 | Vizuri |
| 5 | Uhakiki wa Fasihi Andishi - Riwaya | 1 | 78.6 | Vizuri | 1 | 46.7 | Vizuri |
| 6 | Matumizi ya Lugha katika Miktadha mbalimbali | 1 | 64.5 | Vizuri | 3 | 46.6 | Vizuri |
| 7 | Uhakiki wa Fasihi Andishi - Tamthiliya | 1 | 93.8 | Vizuri | 1 | 45.4 | Vizuri |
| 8 | Kutunga Kazi za Fasihi | 1 | 30.3 | Wastani | 1 | 36.8 | Wastani |
| 9 | Matumizi ya Sarufi | 4 | 59.5 | Vizuri | 2 | 36.3 | Wastani |
| 10 | Maendeleo ya Kiswahili | 1 | 33.9 | Wastani | 1 | 27.7 | Hafifu |

**KIAMBATANISHO B**

## ULINGANIFU WA UFAULU KWA MADA KWA MWAKA 2014 NA 2015

